1.

# ATHARI ZA SIASA KA TIKA KUKUZA LUGHA YA KISWAHILI WILA YANI KABALE NCHINI UGANDA

NA

OWOYESIGANICHORUS
2018/KED/0186/F

TASNIFU ILIYOWASILISHWA KATIKA TAASISI YA LUGHA, KIIIVO CHA ELIMU KUTIMIZA BAA DHI YA MAHITAJI YA KUHITIMU SHAHADA YA ELIMU KATIKA CHUO KIKUU CHA KABALE.

MACHI, 2023

'i

## UNGAMO

Mimi Owoyesiga Nichorus narnbari ya usajili 2018/KED/0186/F, naungarna kuwa utafiti huu wenye rnada ya "athari ya siasa katika kukuza lugha ya Kiswahili wilayani Kabale, nchini Uganda ni wangu mwenyewe na haujawahi kuwasilishwa na mtu yeyote katika chuo kikuu chochote kwa ajili ya kutosheleza rnahitaji ya kuhitirnu shahada yoyote.

Sahihi ..... .

**OWOYESIGA NICHORUS**

**(Mtahiniwa)**

Tarehe
05/05/23

**IDHINI**

Kazi hii ya utafiti imekubalika katika taasisi ya lugha ya Kiswahili, kwa idhini ya msimamizi wa Chuo kikuu cha Kabale.

……

Saini……

**DK. MUTENYO AIDAH**

(Msimamizi)

**SHUKRANI**

Kwanza kabisa, natoa shukrani zangu kwa mwenyezi Mungu kwa kunijalia uzima na kunipa uwezo wa kukamilisha utafiti huu. Asifiwe daima na milele!

Pili, namshukuru sana msimamizi wangu Dk. Mutenyo Aidah kwa kukubali kusimamia utafiti huu mbali na majukumu mengine aliyo nayo, ametumia busara na uvumilivu mkubwa hadi kufika hatua ya kukamilisha utafiti huu. Ahsante sana, nakuombea baraka za mwenyezi mungu tu.

Pia nawashukuru sana Wahadhiri wangu wa Kiswahili katika Chuo kikuu cha Kabale hasa Profesa Ruth Mukama, Dk. Majaliwa David, Bw. Innocent Agume, Bw. Agaba Innocent, Bi. Tusiime Medius Mungu awapatie baraka zake.

Mwishoni nashukuru wazazi wangu Bw. Kabahigye Vito na Bi. Kyenderesire Teodozio kwa kunipa msingi bora na kunielekeza hadi kiwango cha chuo kikuu katika shahada ya ualimu, Mungu awabariki sana. Pia, ni ndugu zangu Bw. Katariwa Tarasi na Mucureezi Linus na dadangu Orikiriza Angela kwa shughuli zote walizonifanyia, naomba mungu awajalie maisha mema na uzima wa milele. Marafiki zangu wote walioniombea na kunitakia ufanisi katika shughuli hii za utafiti nawaombea Baraka kwa mwenyezi.

·Ap

# YALIYOMO

UNGAMO ..... i

IDHINI ..... ii

**SHUKRANI ..... iii**

Y ALIYOMO ..... iv

SURA YA KWANZA ..... 1

UT ANGULIZI ..... 1

I.I Usnliwamada ..... 1

1.2 Suala la utafiti ..... 5

1.4 Maswali ya utafiti ..... 6

1.5 Upeo wa utafiti ..... 6

1.6 **Umuhimu wa** utafiti ..... 6

1. 7 Changamoto zinazotarajiwa na mtafiti ..... 7

1. 8 Maelezo ya istilahi muhimu ..... 8

SURA YA PILI ..... 9

MAPITIO YA MAANDISHI ..... 9

2.1 Utangulizi ..... 9

2.2 Mapitio ya maandishi kuhusu umuhimu wa siasa katika ukuzaji na uendelezaji wa lughaa ya kiswahili. 9

SURA YA TATU ..... 12

3.1 Utangulizi ..... 12

3.2 Mpangilio wa utafiti ..... 12

3.3 Lengo ..... 12

3.4 Eneo ..... 12

3.5 **Mbinu** yaMahojiano ..... 13

3.5.1 Uteuzi wa wahojiwa ..... 13

3.6 Uteuzi wa vifaa ..... 14

3.6.1 Mbinu ya hojaji ..... 14

3.4 Uteuzi wa srunpuli ..... 14

3. 7 Mbinu ya upekuzi wa matini ..... 16

3. 7.1 Matumizi ya tovuti ..... 16

3.8 Utaratibu wa utafiti ..... 16

SURA *YA* NNE ..... 18

2.

UW ASILISHAJI NA UCHANGANUZI WA DAT A ..... .....18
4 .1 Utangulizi ..... .....18
4 .2Tathmini ya hojaji za wanasiasa ..... .....18
U chunguzi shirikishi ..... ..... 2 4
SURA YA T ANO ..... .....25
MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO ..... .....25
5.1 Utangulizi ..... ..... .....25
5.2 **Muhtasari** ..... ..... ..... .....25
5.3 Hitimisho ..... ..... ..... 26
MAREJEO ..... ..... ..... 28

3.

# SURA YA KW ANZA

# UTANGULIZI

## 1.1. Usuli wa mada

Lugha ya Kiswahili ni moja wapo wa lugha zinazotumiwa nchini Uganda. Kuna lugha zaidi ya arobaini ambazo zinatumiwa nchini Uganda, miongoni mwazo kuna za asili na zisizo za asili. Zaidi ya hapo, lugha zinazo eleweka nchini Uganda ni miongoni mwa kingereza, Kiswahili, luganda, kinyankore na nyinginezo. Lugha nyingine zitumiwazo ni kama vile Lusoga, RunyoroRutooro, kikonjo, Rufumbira, Lugisu, Lugubala, kikiga miongoni mwa nyingine. Na kwahivyo Kiingereza na Kiswahili ndizo zinazo tumiwa kama lugha Rasmi za taifa.

Lugha ya Kiswahili ilianza kupitishwa mwaka wa elfu mbili na tano (2005 ). Kulingana na katiba ya mwaka elfu moja mia tisa, tisini na tano (1995), lugha ya Kiswahili ni lugha rasmi ya pili ya taifa baada ya kiingereza. Ni lugha ambayo ilitumiwa kwa asilimia chache kulingana na lugha ya kingereza kwasababu ya mambo kadha wa kadha kama vile; idadi ya wataalamu walio halili mandishi ya Kiswahili ilikuwa chache, ukosefu na kampuni za Kiswahili zilizo stahili kuchapisha vitabu, michango ya serikali kuhusu ufundishaji wa lugha ya Kiswahili nchini Uganda ilikuwa

kwa asilimia chache.

Tangu wakati wa ukoloni katika Afrika mashariki na wakati wa uongozi wa raisi wa Uganda Rais Idi Amin Dada na kwa udhalimu wake, lugha ya Kiswahili ilitumiwa sana na wanajeshi ambao walitesa watu mno, jambo ambalo liliwafanya maraia wa uganda wengi kuwa na mtazamo hasi kuhusu lugha hii, hata baada ya upindunzi wa Rais Idi Amini Dada wanauganda walipoteza hamu ya kuendelea na utumizi wa lugha ya Kiswahili mpaka miaka michache iliopita chanzo cha inchi za Afrika mashariki ambacho kilileta umoja wa kufundisha lugha ya Kiswahili pamoja na kuwa na wimbo moja wa afrika mashariki, jambo hili liliwafanya wanaugnda hasa wanasiasa na wenye biashara kuwa na mwinuko mrnoja wa kuturnia lugha ya kiswahili ili kukuza na kuendeleza uchumi na biashara wakitumia lugha huska ya kiswahili

i

l

i

Kulingana na wizara ya elimu iliyotanguliza mtaala mpya mwaka (2020), Kiswahili ilifanywa somo la lazima katika kidato cha kwanza na cha pili sasa katika shule zote nchini Uganda pamoja na kuongeza idadi ya walimu wanaofundisha Kiswahili kulejelea orodha ya serikali. Hili ni miongoni mwa mambo ya kisiasa ambayo iliendeleza ukuzaji wa lugha ya Kiswahili hasa wilayani kabale nchini Uganda.

Kulingana na Rais wa Uganda Yoweri K. Museveni (tarehe 20/machi/2022), katika kamati ya nchi za afrika mashariki mjini Nairobi, alisema kwamba kujiunga kwa jamuhuli wa kongo, kitaendeleza lugha ya kiswahili hasa wilaya ya kabale itaendelea na kukuza lugha ya Kiswahili kwasababu ya kuwa karibu na mpaka wa taifa la Rwanda pamoja na taifa la Kongo.

Rais Yoweri Museveni pia anawashutumu wabunge wakati wa Mwaka wa 2022 katika misingi ya uhuru huko Kololo mjini Kampala Juni, 7, 2022 . Baraza la Mawaziri la Uganda limekubali kupitishwa kwa Kiswahili kama lugha rasmi na kuelekezwa kuwa ni lazima iwe na suala la lazima katika shule za msingi na sekondari. Baraza la Mawaziri lilipendekeza kuwa mafundisho ya lugha ya Kiswahili katika msingi na sekondari inapaswa kufanywa kwa lazima . Pia ilikubaliwa zaidi kuwa mipango ya mafunzo ya bunge. Kiingereza imekuwa lugha rasmi ya Uganda tangu uhuru mwaka wa 1962. Kifungu kilipendekezwa kama lugha ya pili rasmi mwaka 2005 lakini inafundishwa tu kama somo la hiari katika shule za sekondari tangu mwaka 2017. Wakati wa Kiswahili ni Lingua Franca, akizungumza sana Tanzania kama lugha ya kitaifa na rasmi, ilipitishwa kama lugha rasmi mwaka 2017. Nchi za wanachama wa jumuiya ya Afrika Mashariki ni Tanzania, Kenya, Uganda, Rwanda, Burundi, Sudan Kusini na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo

Aliongeza na kusema tuliteseka wakati wa ukoloni si kwa kuwa babu zetu walikuwa dhaifu lakini kwa kuwa walikuwa wavivu, sisi tuna *uwezo* mwingi tukiungana mikono hivyo tunala kukuza 1 ugha yetu ya kiafrika .

Naibu wa pili wa Waziri mkuu, waziri wa mambo ya jamii ya Afrika mashariki na mwenyekiti wa baraza la mawaziri wa jamii ya Afrika mashariki Bw. Kirunda Ali Kivejinja (2017), alionyesha haja ya lugha ya Kiswahili kukuzwa na kutumiwa kama chombo cha kuleta umoja na kukuza na kuendeleza watu wa Afrika mashariki na pia Bw. Kivejinja alisema kwamba ni kupitia matumizi ya lugha ya Kiswahili kama chombo cha kuunganisha kanda la Afrika mashariki na kuendeleza

4.

lugha ya Kiswahili katika mataifa haya. Waziri katika kufungwa kwa mkutano wa kwanza wa tume la Kiswahili la Afrika mashariki aliendelea na kusema kwamba lugha ya kiswahili ni miongoni mwa lugha zitakazo endeleza uchumi wa taifa la uganda hasa wilaya kama Kabale iliyo karibu na mipaka ya taifa mbili za afrika mashariki yaani Rwanda na karibu najamhuri ya kongo.

Washiriki (wanasiasa) kutoka mkutano huo walionyesha haja ya kufuatilia haraka uanzishaji wa baraza za kitaifa na vyarna vya kitaifa katika nchi zote zinazojenga jamii ya Afrika mashariki, utumiaji na ufundishaji wa lugha ya Kiswahili katika viwango mbalimbali vya elimu, kuunganisha lugha ya Kiswahili katika masomo ya watu wazima wa jamii na pia kuendeleza utafiti wa Kiswahili.

Bi. Rebecca Alitwala Kadaga (2021) ambaye ni naibu wa kwanza wa Waziri Mkuu nchini Uganda alikutana na Asiimwe Caroline, Mhadhiri wa Chuo kikuu cha Makerere kuhusu mambo ya kuweka lugha ya Kiswahili katika mpango wa taifa wa ushirikiano wa kikanda na maendeleo endelevu, hii ni miadi iliyoendelezwa na serikaJi ya Uganda kupitia utafiti wa vyuo vikuu na mtafiti aliliona kama suala litakalo endeleza lugha ya kiswahili wilayani Kabale kwasababu ya kuwa karibu na taifa mbalimbali za afrika mashariki. Uganda ni moja wapo wa nchi zinazojenga jamii ya Afrika mashariki na kuna lengo la kufanya Kiswahili lugha rasmi ya taifa ili kuendeleza ukuzaji wa uchumi, alieleza mawazo kama;

- Raja ya kufanya utafiti
- Kufundisha lugha hii kutoka shule za msingi
- Kutumia lugha ya Kiswahili katika afisi rasmi na mikutano rasmi yote.

Bi. Kadaga alimshukuru sana Bi. Asiimwe kwa ujuzi wake na kupenda kueneza lugha ya Kiswahili nchini kokote, waziri Kadaga a1imhakikisha mhadhiri Asiimwe kwa kusema "nitafuatilia mawazo haya na kukutana na watu waziri husika wa sekta ya elimu, uchumi na biashara.

Kulingana na Ofwono Opondo (2019), "wanauganda wote wanaigwa kuanza kujifunza lugha ya Kiswahili.

Daktari Chris Baryomunsi, Waziri wa habari Mawasiliano Teknolojia na Mwongozo wa Taifa aliidhinisha utekelezaji wa Maelekezo ya Kiswahili na Mkutano wa Jumuiya ya Mashariki ya Afrika Mashariki ambayo Kiswahili kimekubaliwa kama lugha rasmi ya jamii. Uganda sasa ina lugha yaani Kiswahili .

Jumuiya ya Afrika Mashariki huleta pamoja nchi saba za wanachama ikiwa ni pamoja na Uganda, Tanzania, Kenya, Rwanda, Burundi, Sudan Kusini na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo. Baryomunsi alisema Baraza la Mawaziri pia lilielekeza kwamba mafundisho ya lugha ya Kiswahili katika shule za msingi na za sekondari zinapaswa kufanywa lazima na kuzidi . Hiki kitaleta maendeleo katika wilaya zinazokabiliana na hizi nchi Kama Kongo na Rwanda hasa Wilaya ya Kabale .

## 1.2 Suala la utafiti

Wilayani Kabale, baadhi ya wanasiasa wamechangia kikubwa sana hasa juu ya ukuaji na uendelezaji wa lugha ya Kiswahili kwa mfano, Waziri David Bahati ambaye ni Waziri wa biashara na viwanda alijitahidi kuinua baadhi ya shule hasa shule ya Mtakatifu Barnarbas Karujanga kwa kuiombea ufadhili wa serikali. Wanafunzi wanaosomea huko sasa wanapata maarifa juu ya lugha hii ya Kiswahili.

Baadhi ya wanakabale waliweza kusema na kuelewa lugha ya Kiswahili ingawa wengi wao hawajui lugha hii, baadhi ya watu hata hawana nia ya kujifunza lugha hii kwa sababu ya ukosefu wa motisha juu ya umuhimu wa lugha ya Kiswahili.

Wilayani kabale, lugha ya Kiswahili kama somo linalofundishwa katika shule zote za upili. Wanajamii walianza kuwa na mtazamo rnzuri kuhusu lugha ya Kiswahili, suala ambalo liliwatia motisha na k:uteka fikra za wasomi wa kiswahili . Wanasiasa nao walianza kuona umuhirnu na mchango wa lugha ya Kiswahili katika uendeJezaji wa uchumi na biashara nchini Uganda hasa wilayani Kabale, pia chanzo cha kuleta amani na umoja katika nchi za Afrika mashariki ndiyo sababu waliibuka na lengo la kukuza lugha ya Kiswahili kupitia siasa wilayani Kabale, nchini Uganda.

Kwahivyo mtafiti alitilia maanani kufanya utafiti kuhusu athari ya siasa katika kukuza lugha ya Kiswahili wilayani Kabale nchini Uganda.

## 1.3 Madhumuni ya utafiti

lengo kuu la utafiti huu ni kuchunguza athari ya siasa katika kukuza lugha ya Kiswahili nchini Uganda, wilayani Kabale.

Madhumuni mahususi ya uchunguzi huu ni;

(a). Kuchunguza mchango wa siasa katika ukuzaji wa lugha ya Kiswahili wilayani Kabale nchini Uganda.

(b). Kubaini iwapo kuna utayari katika siasa kukuza Iugha ya Kiswahili wilayani Kabale, nchini Uganda .

( c ). Kuchunguza changamoto zinazokabiliwa na siasa katika shughuli za kukuza lugha ya Kiswahili nchini Uganda, wilayani kabale.

1.4 Maswali ya utafiti

(a). Je, siasa ina mchango gani katika ukuzaji wa lugha ya Kiswahili nchini Uganda, wilayani Kabale?

(b). je, kuna utayari wa siasa katika ukuzaji na kuendeleza lugha ya Kiswahili nchini Uganda hasa wilayani Kabale?

( c ). Je, ni changamoto gani zinazokabiliwa na wanasiasa katika shughuli za kuendeleza lugha ya Kiswahili nchini Uganda hasa wilayani Kabale?

**1.5** U **peo wa utafiti**

Utafiti huu ulijikita katika kuchunguza athari ya siasa kukuza lugha ya Kiswahili nchini Uganda hasa wilayani Kabale. Utafiti wa nyanjani ulifanyika kwa wanajamii hasa wale ambao wanaohusika katika siasa na wanajamii ambao wana nia katika siasa, utafiti huu ulifanyika kwa watu katika mji wa Kabale na vijiji kama Kitumba na Muyumbu. Mtafiti alichagua kufanya utafiti wake huko kwasababu anajua watu wengi huko ambayo walikuwa wanaweza kumpa ujumbe na matokeo muhimu kwa hivyo, mtafiti anatarajia matokeo halisi na kweli.

Mtafiti aliwashirikisha wahojiwa ishirini (20). Mtafiti alianza kufanya katika pendekezo la utafiti huu katika mwezi wa Juni mwaka uliopita 2022 na alianza utafiti mwenyewe baada ya pendekezo lake kupitishwa na msimamizi wake mwezi wa novemba 2022. Mtafiti alifanya uchunguzi wake kwa muda wa miezi mitaano, kutoka mwezi wa novemba hadi mwezi wa machi, 2023.

**1.6 Umuhimu wa utafiti**

Utafiti huu utamsaidia mtafiti hata na wanajamii hasa wanasiasa kujua nguvu na umuhimu wao katika ukuzaji wa lugha ya Kiswahili nchini Uganda hasa kupa watu mtazamo mzuri kuhusu lugha hii.

Utafiti huu utakuwa wa faida sana kwa mtafiti pia na wadau wa Kiswahili kama vile wasomi wengi hasa wanafunzi wa lugha ya Kiswahili vyuoni ambao watatumia kazi hii kama marejeo ili kuendeleza uchunguzi zaidi juu ya athari ya siasa katika ukuzaji na uendelezaji wa lugha ya Kiswahili nchini Uganda wilayani kabale.

Pia uchunguzi huu utamsaidia mtafiti kuhitimu shahada ya Sanaa na elimu katika chuo kikuu cha Kabale baada ya kumaliza utafiti wake.

Nyingine, utafiti huu utamsaidia mtafiti kujua michango ya wanasiasa kuhusu ukuzaji na uendelezaji wa lugha ya Kiswahili nchini Uganda hasa wilayani kabale.

Mwishoni, utafiti huu utamsaidia mtafiti kuelewa athari ya siasa katika kukuza lugha ya Kiswahili na mambo mengine kama utayari wa siasa katika ukuzaji wa lugha na changamoto zinazokabiliwa na siasa katika ukuzaji wa lugha.

### 1.7 Cbangamoto zinazotarajiwa na mtafiti

K wanza kabisa mtafiti alihitaji pesa nyingi ili kuendeleza utafiti wake, kwa mfano mtafiti alihitaji pesa za kununua karamu na karatasi, kuchapisha kazi ya utafiti, nauli ya kwenda na kurudi nyanjani katika shughuli za uchunguzi. Mtafiti aliepuka chamgamoto hii kwa kuomba **usaidizi kutoka kwa wazazi wake.**

Mtafiti alikumbwa na shida la kutokuwa na nafasi ya kuzungumza na wahojiwa wake ana kwa ana kwa sababu ya hofu ya virusi vya korona ambavyo ni hatari sana. Mtafiti aliepuka shida hii kwa kutumia hojaji ambayo ilikuwa na maswali na mapengo ambamo wahojiwa walijaza majibu yao, na pia kuungana na wengini kwa kuwapigia simu.

Mtafiti alikumbwa na ukosefu wa muda wa kutosha wa kuchunguza na kukusanya data kwa sababu alikuwa na shughuli nyingine kama kusomea mitihani ya mwisho iliyofanyiwa mtandaoni, kufanya mazoea shuleni na kazi nyingine za nyumbani kwa hivyo mtafiti alijaribu kujitolea mhanga katika muda huu iii kutimiza uchunguzi wake.

Mtafiti alipata shida katika ukusanyaji wa data kwa sababu baadhi ya wahojiwa wake wanaweza kuwa hawana ujuzi wa kutosha kuhusu mambo aliyowauliza na mtafiti alikumbwa na ukosefu wa habari/data iliyohitajika. Mtafiti aliepuka shida hii kwa kupata data kutoka watu mbalimbali na kufanya marekebisho baadaye.

Changamoto nyingine ni wanasiasa nchini Uganda wana mtazamo mbaya kuhusu na lugha ya Kiswahili na kwahivyo baadhi yao waliacha kumpa mtafiti data kwani wanahisi kwamba lugha hii ni ya wezi, wadanganyifu na wahuni.

Mwishoni, wanasiasa wa kitumba na muyumbu hawajui matumizi ya lugha ya Kiswahili na kwahivyo rntafiti alilazimishwa kuenda na rntafsiri ambaye anaelewa kikiga na Kiswahili vizuri.

**1.8 Maelezo ya istilahi muhimu.**

Siasa: kulingana na Wikipedia, karnusi elezo huru, siasa ni njia ya kufanya rnaamuzi katika nganzi mbalirnbali za jamii, karna vile rnji, taifa au hata dunia nzirna.

Lugha: kulingana na kamusi ya Tuki 2004, lugha ni mtindo wa mawasiliano kati mtu mmoja na **mwmgme.**

Utafiti: kulingana na kothairi (1985) anasema kuwa utafiti ni utafutaji wa maarifa. Pia anasema kuwa utafiti unaweza kuelezwa kama sayansi na utaratibu unaowasilisha ujumbe muhimu kuhusiana na mada mausui.

5.

# SURA YA PILI MAPITIO YA MAANDISHI

## 2.1 Utangulizi

Sura hii inahusu maandishi yenye uhusiano na mada ya uchunguzi. Katika sura hii, mtafiti aliangalia maandishi ya wataalamu mbali mbali yenye uhusiano na suala la utafiti wake ili kutambua ikiwa siasa ina umuhimu wowote katika ukuzaji wa lugha ya Kiswahili, mtazamo wake katika wanajamii na matumizi ya lugha ya Kiswahili.

## 2.2 Mapitio ya maandishi kuhusu umuhimu wa siasa katika ukuzaji na uendelezaji wa lugha ya kiswahili.

O-fwono Opondo (2019), alisema kwamba serikali ya nchi ya Uganda imeanza baraza la Kiswahili la taifa ambalo litakuwa na jukumu la kuongoza kuanza kwa lugha ya Kiswahili kama lugha rasmi ya pili ya taifa. Akihutubia waandishi wa habari, Opondo alisema kwamba wanainchi wote lazima waanze kujifunza lugha ya Kiswahili. Pia, alisema kwamba baraza la lugha ya Kiswahili nchini Uganda litasaidia kubadilisha mtazamo wa wanaUganda kuhusu lugha ya Kiswahili kupitia elimu, uhamasishaji kwa wanainchi na kukaribisha watalaam wa Kiswahili kutoka nchi nyingine ili kuwaunga mkono.

Chebet Choge (2012), anasema kwamba wanasiasa na serikali katika Afrika mashariki (EAC) ambamo kuna nchi tano; Tanzania, Kenya, Uganda, Burundi na Rwanda wanajaribu kukuza lugha ya Kiswahili kwa kuipitisha kama moja wapo wa lugha rasmi ambazo ni lugha ya Kifaransa, Kiswahili na Kiingereza. Pia, lugha ya Kiswahili ilipitishwa nchi za Tanzania, Congo na Kenya kama lugha rasmi yao au moja wapo wa lugha rasmi ambazo zinatumiwa. Katika nchi za Uganda, Rwanda, comoros, Burundi na Somalia lugha hii inatumika katika miji mbalimbali. Lugha ya Kiswahili inatumika pia katika mashule hasa yale ya msingi nchini Tanzania na Kenya, inafundishwa pia katika baadhi ya mashule nchini Uganda. Katika masomo ya juu, inafundishwa katika vyuo mbalimbali vya Afrika mashariki kama vile chuo cha Makerere, K yambogo, na kabale nchini Uganda, chuo cha Moi, Kenyatta na Nairobi vya Kenya na pia chuo cha Dar-es-salaam, hii ni njia ya kukuza na kueneza lugha ya Kiswahili.

Mazrui ( 1999), alichunguza kuhusu jinsi siasa na serikali vinaweza kukuza lugha ya Kiswahili na anasema kwamba uchaguzi wa lugha ya Kiswahili kama lugha rasmi ya taifa katika Tanzania na Kenya ulikuwa wa kipekee na mshango katika hara la Afrika, bado badala ya kuwa ya maono, uteuzi huu ulikuwa wa kweli kwa sababu Jugha ya Kiswahili ilikuwa tayari *"lingua franca"* katika eneo hii. Kitu kilichokuwa cha maono kilikuwa uamuzi wa TANU (baada chama cha mapinduzi) kuinua lugha ya Kiswahili kwa ujamaa, sera bunifu ya ujamaa ya kujitegemea kwa Arusha katika mwezi wa januari mwaka elfu moja mia tisa, sitini na saba (1967).

Nyerere (1968:231-50) anasema kwamba uhusiano wakati wa lugha na kujitegemea ulikuwa kuthibitisha uzito wa mamlaka ya ujamaa na lugha ya Kiswahili katika nambari ya watu katika bunge ambao hawakusema lugha ya Kiswahili lakini jambo hili lilikuza lugha ya Kiswahili kwa kuwatenga wale ambao walikuwa wasemaji wa lugha ya Kiingereza tu. Katika mwaka wa elfu moja, mia tisa thelathini na tanao (1985), serikali ya moi ilifanya lugha ya Kiswahili somo lazima kwa masomo ya msingi na sekondari nchini Tanzania. Sera hii ya lugha iliimarisha nafasi ya lugha nchini na jambo hili limeanza kukuza na kueneza lugha ya Kiswahili kwa nchi mbalimbali barani Afrika.

Garett Rucks (2016), Koning (2010), Kubota (2008), Nieta (2002), Tedick Walker (1994) na Weinerberg (1982), wanasema kwamba katika mazingira ya masomo ya lugha ambamo tuna vipengele vya mitaala na jinsi ya kuifundisha iii kusaidia katika utelekezaji na kukuza lugha , mambo ya kisiasa jamii vimeonekana kuwa vitu muhimu vya uchunguzi katika uamuzi, msingi ya jamii- siasa ulikuwepo kwa muda mrefu katika uamuzi wa matumizi ya lugha. K wa muda mrefu watafiti walikuwa na wasiwasi kuhusujinsi utamaduni unawekwajuu katika masomo na matumizi ya lugha. Ingawa vitu vya kijamii vinahusiano na mitaala ya lugha na ni muhimu lakini ina changamoto mbalimbali. Kwa hivyo, lazima kuwepo kushirikiana na kuelewana kati ya sekta za siasa, mataasisi na wadau wa lugha.

Prof. PaJamagamba Kabudi (2019), Waziri wa mambo ya kigeni nchini Tanzania ambaye pia ni mwenyekiti wa SADC *(Southern African Development Community)* anaeleza kwamba lugha ya Kiswahili imepitishwa kama lugha rasmi ya jamii hiyo. Lugha hii itakuwa lugha ya kwanza ya mawasiliano ya mdomo kabla ya kupitishwa kama lugha rasmi katika mawasiliano andishi ya

6.

SADC.

Karenga (1997:123), kuhusu kisiasa geografia anaeleza kwamba walichagua lugha ya Kiswahili kuwa ndiyo lugha tamaduni sahihi kwa Afrika-Amerikani kwa sababu tatu; kwanza, lugha ya Kiswahili si ya kikabila, ya pili, lugha hii ni ya tabia kiAfrika *"pan African"* kama sisi hasa waAfrika-Amerikani wanaopenda kujiambatisha kwa Afrika kwa ujumla na si nchi tu. Ya mwisho, anasema kwamba walichagua lugha ya Kiswahili kama jambo/njia ya kujitawala.

# SURA YA TATU

# MBINU ZA UTAFITI

## 3.1 Utangulizi

Sura hii inahusu mpangilio wa utafiti, eneo, lengo na inawasilisha mbinu zilizotumiwa na mtafiti wakati wa kukusanya data. Mtafiti alitumia mbinu mbalimbali ambazo zilimsaidia kukusanya na kupata data muhimu ambayo ilimwezesha kukamilisha utafiti wake. Zifuatazo ni mbinu ambazo mtafiti alitumia kukusanya data; uteuzi wa sampuli, uteuzi wa wahojiwa (mahojiano), uteuzi wa vifaa na utaratibu wa utafiti.

## 3.2 Muundo wa utafiti

Mtafiti alitumia mtindo wa kiuthamano na kiwingi idadi na pia kutumia maelezo katika uchunguzi wake kwa kufafanua dhana mbalimbali. Mtafiti alilenga kupata maelezo ya dhana mbalimbali kutoka wahojiwa wake. Pia mtafiti alitumia mtindo wa kiwingi idadi katika mji wa Kabale na vijiji vya kitumba na Muyumbu. Mtafiti alikuwa na wahojiwa ishirini (20). Mtafiti alitumia vifaa na mbinu mbalimbali kukusanya data kama anavyoeleza hapo chini

## 3.3 Lengo

Lengo kuu la utafiti huu ni kuchunguza athari za siasa katika ukuzaji wa lugha ya Kiswahili kijijini kitumba na muyumbu, wilayani Kabale nchi Uganda. Mchango wa siasa katika ukuzaji wa lugha ya Kiswahili, changamoto zinazoletewa na siasa katika shughuli za ukuzaji wa lugha Kiswahili na kubaini ikiwa kuna ukuzaji wa lugha ya kiswahili katika shughuli za siasa nchini Uganda wilayani Kabale.

## 3.4 Eneo

Utafiti huu ulifanyika kwa wanajamii hasa wale waliohusika katika siasa na wanajamii ambao wana nia katika siasa, utafiti huu ulifanyika kwa watu katika mji wa Kabale na vijiji vyake kama Kitumba na Muyumbu. Hivyo basi ndivyo vijiji mtafiti alichagua kufanyia utafiti wake kwasababu alijua watu wengi hasa wanasiasa wenye uwezo wa kumpa data na masuala muhimu kuhusu mada yake ya utafiti na kwa hivyo, mtafiti alihitaji matokeo halisi na ukweli, lngawa wanajamii walikuwa na mtazamo chanya kuhusu lugha ya Kiswahili kwamba ni lugha ya wahuni, wezi,

wadangayifu na was1o na ma ya kutumia lugha hii. Hata hizo ndizo changamoto mtafiti alizokubaliana nazo katika eneo lake la utafiti wilayani Kabale nchini Uganda.

**3.5 Mbinu ya Mahojiano.**

Mahojiano ni mazungumzo ya ana kwa ana kati ya mtafiti na mhojiwa. Wahojiwa wa mtafiti walikuwa wanasiasa na wanajamii kutoka mji wa Kabale na vijiji vya Kitumba na Muyumbu wilayani Kabale.

Mtafiti alifanya mahojiano na wanajamii ana kwa ana ambapo alimhoji Karekyezi Pakarasio ambaye ni mwenyekiti wa kijiji cha Muyumbu ambapo alimuuliza kama ana ufahamu wowote kuhusu lugha ya Kiswahili, je, ni wanasiasa gani ambao unawafahamu kuhusu uendelevu wa lugha ya Kiswahili wilayani kabale? Ni mchango gani unao jua kuhusu Kiswahili kutoka kwa wanasisa ha.pa wilayini Ka.bale nchini Uganda? Baadaye, Bw. Karekyezi alimjibu kwamba Kiswahili ni lugha inayo fahamika na kutumika mara nyingi kwa wanajeshi pamoja na kufundisha katika shule za upili, tena aliendelea na kudai kwamba ni Mbunge Waziri David Bahati ambaye analipia wanafunzi wanao soma Kiswahili katika shule la upili Mtakatifu Bamarbas Karujanga kama jambo la kukuza na kuendeleza Kiswahili katika wilaya ya Kabale.

Mtafiti alipata muda wa kuwahoji wahojiwa wake wakati wa muda wao wa ziada ili kutoingilia shughuli zao za kazi zao nyingine. Mtafiti aliuliza maswali kwa sauti kuhusu athari ya siasa kukuza lugha ya Kiswahili nchini Uganda.

Mbinu hii ilimsaidia mtafiti kuongea na wahojiwa wake ana kwa na kugawana mawazo nao jambo ambalo lilimsaidia kupata taarifa midi. Kwa kuwa na hofu ya virusi vya korona, matumizi ya barakoa, kunawa viganja na umbali wa mita ndivyo vilivyomsaidia kukusanya data kutoka kwa wahojiwa wake katika vijiji vya wilaya ya Kabale yaani Kitumba na Muyumbu.

**3.5.1 Uteuzi wa wahojiwa.**

Wahojiwa ni watu au vikundi vya kulengwa vya watu ambavyo hutumika kukusanya data kupitia majadiliano au mahojiano katika kikao au mahali fulani.

Wahojiwa waliteuliwa miongoni mwa wanasiasa na wanajamii mbalimbali. Mtafiti alihoji jumla ya wahojiwa ishirini (20) kwa kuchagua kumi kutoka vijiji vya na Kitumba na Muyumbu na wengine kumi kutoka mji wa Kaba.le. Mbinu hii ilimsaidia mtafiti kupata kujua misimamo na mawazo ya

wanasiasa na wanajamii mbalimbali kuhusu athari ya siasa katika kukuza lugha ya Kiswahili nchini Uganda, jambo hili lilimsaidia kutoa hukumu na tathmini yake akitumia matokeo kutoka kwa wahojiwa wake mbalimbali.

### 3.6 Uteuzi wa vifaa

Vifaa ni vyombo ambavyo hutumiwa wakati wa utafiti ili kusaidia mtafiti kukusanya data. Mtafiti alitumia vifaa mbalimbali ambavyo vilimsaidia kupata data na ujumbe wowote muhimu uliohitajika ili kutimiza utafiti wake.

Mtafiti alitumia miongozo ya maswali ya mahojiano kwa wahojiwa wake. Mtafiti alitumia hojaji ili kukusanya data, zana nyingine ambazo zilitumiwa katika ukusanyaji wa data ni Pamoja na dodoso zilizokuwa na maswali kwa wahojiwa huku wakiombwa kuyajaza kwa uwezo wao iwezekanavyo. Vifaa hivi vilimsaidia mtafiti kupata data muhimu ambayo ilimsaidia kukamilisha utafiti wake.

#### 3.6.1 Mbinu ya hojaji

Hojaji ni karatasi yenye mwongozo wa maswali yaliyoundwa na mtafiti kwa wahojiwa wake, wahojiwa huwa wanatarajiwa kujibu maswali hayo kwa kuandika majibu yao katika hiyo karatasi kulingana na maagizo yaliyowapewa na mtafiti.

Mbinu hii ilitumika na mtafiti kwa kuunda hojaji ambayo itakuwa na maswali yaliyokuwa na mpangilio maalum. Mtafiti aliwapa maswali hayo wahojiwa wake na kuwaomba kuyajibu kwa kujaza mapengo na kuyarudisha kwa mtafiti. Seti moja ya maswali ilikuwa ya wanasiasa na nyingine ya wanajamii. Kila kikundi cha wahojiwa waliulizwa mzswali kulingana na uwezo wao. Mbinu hii ilimsaidia mtafiti kupata data kweli kutoka kwa wahojiwa wenyewe (wanasiasa na wanajamii), pia mbinu hii iliwapa wahojiwa uhuru wa kuandika vyote walivyofikiri bila kusumbuliwa na mtafiti. Baada ya kupata majibu ya wahojiwa wote, mtafiti alilinganisha na kutoa tathmini kuhusu suala lake la utafiti.

### 3.7 Uteuzi wa sampuli.

Sampuli ni mbinu ya ukusanyaji data ambayo iliturniwa kwa kuchagua kinasibu vipengele au wahojiwa wachache kutoka idadi ya watu wengi ili kuwakilisha wengine.

Watu kutoka katika wilaya ya Kabale waliteuliwa katika uchunguzi ambapo wanasiasa na wanajamii walihojiwa katika kila Kijiji yaani mji wa Kabale, Kijiji cha kitumba na Muyumbu, mtafiti alichagua wahojiwa kumi (10) kutoka mji wa Kabale, watano kutoka Kitumba na watano pia kutoka Muyumbu. Hivyo basi Serikali ya Uganda imechukua hatua za kukuza na kueneza lugha. Mtafiti alikuwa na wahojiwa ishirini (20) kwa ujumla.

Mbinu hii ilimsaidia mtafiti kuhifadhi rasilimali kama vile muda na vifaa vyingine kama vile pesa za kuchapisha miongozo ya maswali (hojaji).

Maagizo: jibu maswali yafuatayo kwa kujaza mapengo yaliyoachwa.

Jina .....Jina la mahali ..... .

1. Wewe kama mwanasiasa, unafikiri siasa ina athari yoyote katika ukuzaji wa lugha ya Kiswahili, wilayani Kabale, nchini Uganda?

2. Ikiwa jibu lako ni sawa hapo juu, toa athari ya siasa katika ukuzaji wa lugha ya Kiswahili, wilayani Kabale, nchini Uganda.

3. Siasa ina mchango gani katika ukuzaji na matumizi ya lugha ya Kiswahili, wilayani Kabale.nchini Uganda? ...

4. W anasiasa wanakutana na changamoto gani wakati wa kuendeleza matumizi ya lugha ya Kiswahili, wilayani Kabale, nchini Uganda.

… … … …

### 3.8 Mbinu ya upekuzi wa matini.

Mbinu hii inahitaji mtafiti kurejelea kazi andishi za watalaam mbalimbali kwa kusoma matini zao, vitabu na maandishi mengine yanayolingana na mada ya utafiti wake.

Mtafiti alitumia mbinu hii kutafuta data kwa kusoma matini mbalimbali kama vile vitabu teule, majarida na vitabu vya ziada kulingana na malengo ya utafiti wake. Mtafiti pia alijaribu kusoma tasnifu nyingine za wanavyuo ili apate data za kukidhi haja za utafiti wake. Mbinu hii ilimsaidia kupata taarifa nyingi, data muhimu na marejeo, vyote ambavyo vilimsaidia kutimiza utafiti wake kulingana na malengo yake.

#### 3.8.1 Matumizi ya tovuti

Mbinu hii hutumiwa sana mtandao kwa kutumia vifaa mba1imbali kama vile, simu na computa ili kukusanya data/taarifa.

Mtafiti alijaribu kutumia mbinu hii ili kupata data kutoka kwa intaneti kwa mfano ile data ambayo **ilikuwa** nadra kupatikana maktabani na matini nyingine zilizoandikwa na watu mbalimbali. Mtafiti aliweza kupata tasnifu na marejeo mengi kutoka kwa intaneti ambazo zilimsaidia

kuboresha na kufanikisha utafiti wake.

### 3.9 Utaratibu wa utafiti

Mtafiti alianza utafiti wake kwa kuandaa mada ya utafiti yaani'athari ya siasa katika kukuza lugha ya Kiswahili nchini Uganda, wilayani Kabale na kuipeleka kwa msimamizi wake Bibi Aidah Mutenyo ambaye alikubali na kumwambia kuendelea na kuandika pendekezo lake. Baadaye, mtafiti alianza na kusoma matini mbalimbali kuhusu mada yake na yale yenye uhusiano nayo na kuanza kuandika pendekezo lake kwa kutumia barua pepe kwa msimamizi wake ili kupata ushauri kuhusu uendelezaji wa utafiti wake.

Msimamizi alimwambia afanye marekebisho machache katika pendekezo lake, alimpa mwelekeo, mashauri na kumwambia kuendelea na uchunguzi mwingine wowote uliohitajika na piakukusanya na kuandika ripoti ya utafiti.

Kutoka hapo, mtafiti alienda nyanjani kukusanya data kwa mfano alienda mahali tofauti kuwahoj i wahojiwa, akitumia mbinu na vifaa mbalimbali kama alivyoeleza hapo awali. Baada ya kusaka data. mtafiti a1iwasilisha na kuichanganua akitumia maonyesho kutoka kwa wahojiwa wake na

ukweli mwingine kutoka uwanjani. Kisha mtafiti alitoa muhtasari wa utafiti wake, hitimisho na mapendekezo yake na kuipeleka ripoti ya utafiti kwa msimamizi wake Dkt. Mutenyo Aidah kuithibitisha.

## SURA YANNE

## UW ASILISHAJI NA UCHANGANUZI WA DATA 4.1

**Utangulizi**

Katika sura hii, mtafiti aliwasilisha na kuchanganua uchunguzi wake wa data ambayo alifanikiwa kupata kutoka uwanjani kwenye eneo lake la utafiti baada ya kuwasilisha Pamoja na kutumia mbinu zake mwafaka ambazo alionyesha hapo awali katika sura ya tatu.

Katika utafiti huu, mtafiti alichagua shule na vijiji vya Muyumbu na Kitumba na pia mji wa Kabale. Mtafti alitumia jumla ya wahojiwa ishirini (20) yaani wanasiasa na wanajamii kwa kuchagua kumi kutoka mji wa Kabale, na watano kutoka Kijiji cha Muyumbu na pia watano kutoka Kitumba. Wakati wa kutathmini, mtafiti alitumia hati (A) kuwasilisha mji wa Kabale, hati (B) kuwasilisha Kitumba na hati (C) kuwasilisha Muyumbu.

**4.2 Tathmini ya hojaji za wanasiasa.**

Mtafti alihoji wanasiasa kutoka mji wa Kabale. Lengo kuu la hojaji ya wanasiasa lilikuwa kupata data kuhusu mawazo yao katika mchango wa siasa katika ukuzaji wa lugha ya Kiswahili wilayani Kabale nchini Uganda.

Wanasiasa walipoulizwa na kuhojiwa kuhusu kwamba wanafikiri siasa ina athari yoyote katika kukuza lugha ya Kiswahili wilayani Kabale nchini Uganda ilibainika kwamba wanasiasa watano wote walithibitisha kwamba siasa ina mchango mkubwa katika ukuzaji wa lugha yoyote kama Kiswahili kwa sababu serikali kupitia siasa yake huwa na jukumu la kutekeleza masuala yote katika nchi.

**Mtafiti aliwauliza wanasiasa maswali yafuatayo:**

Je, unafikiri siasa ina athari yoyote katika kukuza lugha ya Kiswahili nchini Uganda? **Jedwali 1** linaonyesha majibu ya wanasisa kuhusu mchango wa siasa katika kukuza lugha ya Kiswahili nchini Uganda ambayo yameonyeshwa kwa asilimia

| **Asilimia** (%) | **Idadi ya wanasiasa** |
|---|---|
| Chini ya asilimia thelathini (30) | Mwanasiasa mmoja (01) |
| Asilimia thelathini hadi asilimia hamsini (30-50) | Mwanasiasa mmoja (01) |
| Zaidi ya asilimia hamsini (50) | Wanasiasa watatu (03) |

lil

J edwali hii linaonyesha kwamba wanasiasa wengi yaani asilimia sitini ( 60%) wanafikiri kwamba siasa ina mchango mkubwa katika ukuzaji na uendelezaji wa lugha ya Kiswahili wilayani Kabale nchini Uganda na mwanasiasa mmoja ndiye anafikiri kwamba siasa huna mchango mchache yaani chini asilimia thelathini (30%)

**Je, unadhani kwamba wanasiasa wana uwezo wa kusaidia katika ukuzaji na uendelezaji wa lugha ya Kiswahili?**

**Jedwali 2** linaonyesha maoni ya wanasiasa kuhusu uwezo wao kwa kusaidia katika ukuzaji wa lugha ya Kiswahili nchini Uganda wilayani Kabale.

| **Maoni** | **Wanasiasa kutoka mji A** | **Asilimia** (%) |
|---|---|---|
| Ndiyo | 04 | 80 |
| Hapana | ……. | 00 |
| Sijui | 01 | 20 |
| Jumla | 05 | 100 |

Asimilia kubwa ya themanini walikubali kwamba wanasiasa wana uwezo wa kukuza na kuendeleza lugha ya kiswahili wilayani Kabale nchini Uganda na wanasiasa hawa walisema kwamba wana ushawishi mkubwa kwa wanajamii na wanaweza kuwapendesha lugha hii hasa wale ambao wana mtazamo mbaya kwa lugha hii, pia walisema kwamba waweza kushawishi serikali kuwapa rasilimali muhimu zinazohitajika kukuza na kuendeleza lugha ya Kiswahili nchini Uganda kwani ndiyo wanaendeleza mawazo yote ya serikali.

Asilimia ishirini (20) ya wahojiwa walisema kwamba hawajui ikiwa wanasiasa wana uwezo wa kusaidia katika kukuza na kuendeleza lugha ya Kiswahili wilayani Kabale nchini Uganda. Kulingana na maoni ya wanasiasa waliohojiwa katika jedwali la hapo juu, wanasisa wana uwezo wa kusaidia katika ukuzaji na uendelezaji wa lugha ya Kiswahili nchini Uganda.

**Je, siasa ina athali gani katika kukuza na kuendeleza lugha ya Kiswahilii** wilayani Kabale nchini Uganda?

**Jedwali 3** linaonyesha rnaoni ya wanas1asa na wanajarnii (wahojiwa) kuhusu jinsi siasa inaweza kusaidia katika ukuzaji wa lugha ya Kiswahili nchini Uganda.

| **Maoni** | **Wahojiwa kutoka mji A** | **Wahojiwa kutoka Kijiji B** | **Wahojiwa kutoka Kijiji C** | **Jumla (/20)** | **Asilimia (%)** |
|---|---|---|---|---|---|
| Ukuzaji wa lugha katika mashule na elimu nchini. | 8 | 5 | 4 | 17 | 85 |
| Kutekeleza uturniaji wa lugha mikutano rasmi | 5 | 5 | 5 | 15 | 75 |
| Kuwekeza katika vifaa vinavyohitajika kukuza lugha | 6 | 5 | 5 | 16 | 80 |
| Kukuza utumiaji wa lugha katika ofisi zote nchini | 10 | 5 | 5 | 20 | 100 |

Kwa kurejelea aasilimia za hapo juu, jedwali hili linaonyesha kwamba watu wengi waliohojiwa walikubali kwamba siasa inaweza kukuza lugha ya Kiswahili wilayani Kabale nchini Uganda, majibu yao yalikuwa kwamba'siasa *inasaidia kwa ukuzaji wa lugha kupitia mashule na elimu nchini, kutekeleza utumiaji wa lugha katika mikutano rasmi yote, kuwekeza katika vifaa vinavyohitajika kukuza lugha na kukuza utumiaji wa lugha katika ofisi zote rasmi'* kama vinavyoonyeshwa katika jedwali la hapo juu.

K wa hivyo, kulingana na majibu yaa hapo juu, siasa inaweza kusaidia katika kukuza lugha ya Kiswahili wilayani Kabale nchini Uganda

Je, unadhani kwamba kuna utayari wowote katikaa siasa kukuza lugha ya Kiswahili nchini Uganda?

**Jedwali** 4 linaonyesha majibu ya wahojiwa ikiwa siasa ina utayari wowote katika ukuzzaji wa lugha ya Kiswahili wilayani Kabale nchini Uganda.

| majibu kutoka kwa wahojiwa | MjiA | Kijiji B | Kijiji C | Asilimia (%) |
|---|---|---|---|---|
| Ndiyo | 8 | 4 | 5 | 85 |
| Hapana | … … …. | 1 | ……. | 05 |
| Sijui | 2 | … … … . | ……. | 10 |
| Jumla | 10 | 5 | 5 | 100 |

Kulingana na jedwali la hapo juu, asilimia themanini na tano (85%) ya wahojiwa walikubali na kusema kwamba siasa ina mchango na utayari kukuza lugha ya Kiswahili nchini Uganda. Mhojiwa mmoja (mwanasiasa) kutoka kijiji B alisema kwamba serikali kupitia siasa yake imekwisha na kuanza kukuza lugha ya Kiswahili kupitia elimu na masomo katika mashule yote **nchini Uganda, mhojiwa aliendelea *kusema'katika*** *mashule yote ya msingi na ya upili, Kiswahili ilipitishwa mwaka wa 2020 kwa moja wapo wa masomo ambayo lazima yasomwe na wanafunzi wote katika mashule ya Uganda hasa wilayani Kabale*."

Asilimia tano (05%) tu ya wahojiwa yaani 1/20 ndiye alisema kwamba siasa sio tayari kukuza lugha ya Kiswahili nchini Uganda, yeye analinganisha Uganda na nchi nyingine katika afrika mashariki hasa Tanzania ambayo asilimia kubwa ya watu wanaweza kusema na kutumia Kiswahili wakati wowote na kusema wanasiasa wa Uganda hawawezi kuendeleza kitu chochote nchini humu hasa lugha ya Kiswahili. Asilimia kumi (10%) ya wahojiwa walisema kwamba hawajui kwamba siasa ina utayari wa kukuza lugha ya Kiswahili wilayani Kabale nchini Uganda.

Hivyo basi, kulingana na majibu ya wahojiwa, siasa ina uwezo na utayari wa kukuza na kuendeleza lugha ya Kiswahili nchini Uganda wilayani Kabale.

**Je, ni changamoto gani zinazokabiliwa na siasa katika kukuza lugha ya Kiswahili nchini Uganda wilayani Kabale?**

**Jedwali 5** linaonyesha maoni ya wahojiwa katika changamoto zinazokabiliwa na siasa katika shughuli za kukuza lugha ya Kiswahili wilayani Kabale nchini Uganda.

| **Changamoto zinazokabiliwa na siasa katika shughuli za kukuza lugha ya kiswahili** | **Maoniya wahojiwa kutoka Kijiji A** | **Maoniya waahojiwa kutoka Kijiji B** | **Maoniya wahojiwa kutoka Kijiji C** | **Asilimia (%)** |
|---|---|---|---|---|
| Ukosefu wa rasilimali za kuendeleza lugha | 7 | 3 | 1 | 55 |
| Ushindani kutoka lugha za kitamaduni na viongozi vya kitamaduni | 8 | 5 | 5 | 90 |
| Kutopewa nafasi ya kutumiwa nyanjani mbalimbali kama lugha ya kiingereza. | 10 | 5 | 4 | 90 |
| Mtazamo mbaya wa watu kuhusu **lugha ya kiswahili** | 9 | 5 | 3 | 85 |

Jedwali hili linaonyesha kwamba wahojiwa wengi yaani 18/20 wanakubali kwamba lugha ya Kiswahili umekumbwa na ushindani kutoka viongozi vya kitamaduni na pia lugha nyingine za kitamaduni hasa Luganda, Runyoro na nyinyine ambamo watu hawajaona sababu ya kubadilisha ukuzaji wa lugha zao kwa Kiswahili ambayo wanaita lugha ya kigeni.

Wengine, yaani asilimia (90%) walisema kwamba katika shughuli za kukuza lugha ya Kiswahili, kuna changamoto ya lugha kutopewa nafasi ya kutumiwa nyanjani mbalimbali kama lugha mbalimbali, sababu hii ni kwamba kufikiria kwamba watu wengi nchini hawaelewi
lugha ya Kiswahili.

Wahojiwa 17/20 yaani asilimia themanini na tano (85%) walisema uendelezaji na ukuzaji wa lugha ya Kiswahili umekumbwa na mtazamo mbaya wa watu kuhusu lugha ya Kiswahili ambao umewafanya kutokuwa na nia ya kujifunza au kutumia lugha hii. Mhojiwa mmoja kutoka Kijiji B alisema kwamba 'lugha ya Kiswahili ni lugha ya wanajeshi, ukiitumia watu wengi watafikiri kuwa wewe ni mwanajeshi, polisi au askari, lugha ilikuwa inatumiwa na

wahuni, wezi, wadanganyifu na wajanja jambo ambalo limewafanya watu wengi kutokuwa na nia ya kujifunza hii lugha au kuitumia Nyanja mbalimbali'

Kwa hivyo, wanasiasa na wataalam wa lugha ya Kiswahili wana jukumu kubwa katika ubadilishaji wa mitazamo mbaya ya wanajamii kuhusu lugha ya Kiswahili kupitia elimu.

**Je, unafikiri kwamba changamoto zinazokabiliwa na wanasiasa na wataalam wa Kiswahili zinaweza kutatuliwa vipi?**

**Jedwali 6** linaonyesha majibu ya wahojiwa kuhusu jinsi changamoto zinazokabili ukuzaji wa lugha ya Kiswahili zinaweza kutatuliwa.

| **Azimio** | **Wahojiwa kutoka mji A** | **Wahojiwa kutoka Kijiji B** | **Wahojiwa kutoka Kijiji C** | **Asilimia (%)** |
|---|---|---|---|---|
| Ufundishaji wa lugha ya Kiswahili kwa mashule | 10 | 5 | 5 | 100 |
| Ufundishaji wa lugha katika redio na runinga | 9 | 4 | 5 | 90 |
| Uhamasishaji jamii kuhusu umuhimu wa lugha ya Kiswahili na mchango wake katika uchumi | 10 | 5 | 4 | 95 |
| Kuendeleza matumizi ya Kiswahili katika ofisi na mikutano rasmi | 7 | 3 | *5* | 75 |

Kulingana na jedwali la hapo juu, watu wote waliohojiwa na mtafiti walisema kwamba kufundisha lugha ya Kiswahili katika mashule ya msingi na sekondari ni njia bora ya kukuza na kuendeleza lugha ya Kiswahili. Mhojiwa mmoja kutoka Kijiji A alisema kwamba *'asilimia kubwa ya vijana nchini Uganda ni wanafunzi na ikiwa wanajua kutumia lugha ya kiswahili, walimu wao wakibadilisha mtazamo wao kuhusu lugha ya Kiswahili lazima watatusaidia kuieneza nchini kokote*'

Wahojiwa yaani 18/20 pia walisema kwamba ufundishaji wa lugha ya Kiswahili katika redio na runinga unaweza kusaidia wanaUganda wengi kujifunza na kupenda lugha ya Kiswahili ila wawili 2/20 ambao walisema kwamba kuna watu ambao hawana redio na runinga, mmoja wapo kutoka Kijiji C alisema kwamba watu wengi wa wilaya ya kabale nchini Uganda ni maskini, hawana redio au runinga na kwa hivyo hawawezi kujifunza lugha ya Kiswahili au kujua umuhimu wake kupitia vyombo hivyo, wengine ambao ndio walikuchukua asilimia kubwa ya wanaUganda ni walimi ambao hawana muda wa kusikiliza redio na kuwa kwa televisheni hasa wakati wa mchana

Wahojiwa wengine walisema kwamba wanasiasa na watalaam lazima waanze kuhamasisha wanajamii kuhusu umuhimu wa lugha ya Kiswahili na mchango wake katika ukuzaji na uendelezaji wa uchumi wa Uganda na taifa nyingine za Afrika mashariki.

**Uchunguzi shirikishi**

Mtafiti alishiriki nyanjani yeye mwenyewe kwa ajili ya kujionea ikiwa siasa ina athari katika ukuzaji wa lugha ya Kiswahili wilayani Kabale nchini Uganda kwa kujiunga na kuwa na wanajamii rnbalirnbali kutoka vijiji vya wilaya ya Kabale yaani Kiturnba na Muyurnbu, kwa watu kumi ambao rntafiti alishiriki nao watatu (3) ndio walikuwa wanaweza kuserna sentensi au rnaneno ya lugha ya kiswahili ambazo wengine walikuwa na ukosefu wa kisarufi. Wanajamii wengi sana walikuwa hawawezi kusema zaidi ya maneno mawili katika lugha ya Kiswahili.

Mtafiti pia aligundua kwamba baadhi ya wanasiasa hawajui kwamba ushirikaji wao ni muhimu sana katika kukuza na kuendeleza lugha hasa Kiswahili wilayani kabale nchini Uganda. Jambo hili limeifanya Kiswahili kutokuwa na nafasi ya kujulikana kama lugha muhimu katika rnahali mbalimbali nchini Uganda kwa sababu hata viongozi wenyewe hawajui umuhimu wa lugha hii. Viongozi ndio wanaweza kushawishi wanajamii wengine kuwa lugha ya Kiswahili ndio lugha yetu kabisa ambayo inaweza kuleta urnoja katika bara la Afrika, kwa hivyo wanasiasa wanafaa kutumia nafasi zao kuwatia rnotisha wengine kwa kutumia lugha ya Kiswahili na pia kuhamasisha wale ambao wana mtazamo mbaya katika ukuzaji na uendelezaji wa lugha ya Kiswahili.

# SURA YATANO

## MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

### 5.1 Utangulizi

Sura hii inashughulikia muhtasari, hitimisho na mapendekezo kulingana na maoni na matokeo ya utafiti uliofanywa.

### 5.2 Muhtasari

Utafiti huu wenye mada'athari ya siasa katika kukuza lugha ya Kiswahili wilayani Kabale nchini Uganda' ulifanywa na malengo yafuatayo:

7. Kuchunguza mchango wa siasa katika ukuzaji wa lugha ya Kiswahili nchini Uganda.

8.Kubaini iwapo kuna utayari katika siasa kukuza lugha ya Kiswahili hasa wilayani Kabale nchini Uganda.

3. Kuchunguza changamoto zinazokabiliwa na siasa katika shughuli za kukuza lugha ya Kiswahili wilayani Kabale nchini Uganda.

Vijiji katika wilaya ya Kabale ndivyo vilichaguliwa katika utafiti huu yaani mji wa Kabale, vijiji vya Kitumba na Muyurnbu. Wanasiasa Pamoja na wanajamii ndio walikuwa wajibu wa mtafiti, mtafiti alihoji jumla ya wahojiwa ishirini (20), wanasiasa kumi (10) kutoka mji wa Kabale, na wanajamii kumi (10) kwa kutoa watano (5) kutoka Kijiji cha Muyumbu na watano ( 5) wengine kutoka Kijiji cha Kitumba. Mtafiti alitumia mbinu mbalimbali za kukusanya data ambazo ni Pamoja na uteuzi wa sampuli, uteuzi wa wahojiwa, uchunguzi shirikishi, upekezi wa matini, matumizi ya tovuti. Mbinu hizi ndizo zilimsaidia kupata ujumbe uliohitajika kutimiza utafiti wake.

Kulingana na utafiti huu, wanajamii wachache ndio wanaweza kutumia na kusema lugha ya Kiswahili, kwa upande mwingine wale ambao hawawezi kutumia wala kusema lugha ya Kiswahili ndio wengi yaani asilimia 70% ya watu waliohojiwa

Pia **wanasiasa** wengi waliohojiwa yaani aslimia 60% ya wote waliohojiwa walisema kwamba wao hawawezi kutumia au kusema Kiswahili vizuri, asilimia sitini ( 60%) pia walisema kwamba wahajashiriki katika mawazo ya ukuzaji wa lugha ya kiswahili katika mahali yao.

t

~ ~

Kutokana na maoni ya wahojiwa siasa ina mchango mkubwa katika ukuzaji na uendelezaji wa lugha ya Kiswahili nchini Uganda.

Siasa inaathiri karibu vitu na kazi zote zinazoendelea katika nchi kulingana jinsi wanaendeleza mawazo yao, siasa katika serikali yake yaweza kushawishi watu kupenda na kutumia lugha kwa kutia motisha wanajamii, kuwahamasisha kujifunza lugha ya Kiswahili, na kuendeleza utumiaji na ufundishaji wa lugha ya Kiswahili katika viwanda mbalimbali kama vile mikutano rasmi, ofisi na mashule.

K wa hivyo, siasa ni chombo muhimu sana kinachoweza kusaidia katika kukuza lugha ya Kiswahili, wanasiasa na watalaam wa Kiswahili wanafaa kutumia nafasi zao kwa kukuza na kueneza lugha ya Kiswahili nchini kokote hasa wiliya ya Kabale.

5.3 Hitimisho

Wanajamii na wanasiasa waliohojiwa wote walikubali kwamba siasaa ina athari kubwa katika ukuzaji, uendelezaji na utumiaji wa lugha ya Kiswahili wiyani Kabale nchini Uganda ingawa baadhi ya wanasiasa waalikuwa hawajui jukumu lao katika kukuza lugha hii katika nchi hasa wanasiasa wa wilaya ya Kabale.

Mtafiti alihitimisha kwamba siasa ina athari kubwa katika ukuzaji wa lugha ya Kiswahili na wanasiasa wanafaa kutumia nafasi zao kuendeleza hii lugha.

## 5.4 Mapendekezo

Wanasiasa nchini Uganda wanafaa kutumia uwezo wao kuwatia motisha na kuwahamasisha wanajamii ambao wanamtazamo mbaya kwa lugha, kutumia lugha ya Kiswahili kupitia kuwaonyesha umuhimu wa lugha hii kwa nchi na masoko ya Afrika mashariki na pia sekta nymgme.

Wataalam wa Kiswahili wanafaa kushawishi baadhi ya wanasiasa ambao wana mtazamo mbaya kuhusu lugha ya Kiswahili, kuwaonyesha umuhimu wa lugha ya Kiswahili kwa nchi ya Uganda na kwa ukuzaji wa uchumi wa nchi hii. Pia wanasiasa wana akili kwa lugha ya Kiswahili kuwa moja wapo wa lugha zitazotumiwa kirasmi.

Wanasiasa wanafaa kufanya chochote wanachoweza kufanya ufundishaji wa lugha ya Kiswahili katika rnashule ya viwango rnbalirnbali kuwezekana katika upatikanaji wa rasilirnali rnuhirnu.

## MAREJEO


Mulokozi, MM (2000), language, literature and the forging of Pan African identity. Kiswahili: Journal of the institute ofKiswahili research 63: 71-81, university of Dar-es-Salaam.

Dr. Mwenda Mukuthuria (2006), Kiswahili and its expanding roles of development. Nordic journal of African studies 15(2): 154-165

New error newspaper, August 17, 2019

Mazrui Ali A. ana Alamin M, Mazrui ( 1999), Political culture of language: Swahili society and state, Binghamton: institute of Global Cultural Studies, 2" edition.

Nyerere Julius K (1968), Freedom and socialism, Uhuru na Ujamaa. A selection from writings and speeches 1965-67, Dar es Salaam: Oxford press.

http://WWW.africareview.com/special-reports/why-kiswahili-has-taken-off-in-**uganda/979182-1760180-pwk8rwz/index.htm1**

Uganda's presidential speech at the Kololo independence grounds in Kampala on June 04, 2021

East Africa Kiswahili Commission Journal, 08 September, 2017, Zanzibar Tanzania.